**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**
**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA, 2024) ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA LEWIS KALINJUNA TAREHE 31.10 - 01. 11.2024**

## A. WAJUMBE

**WALIOHUDHURIA:**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Elias R. Masumbuko | Mstahiki Meya (Mwenyekiti) |
| 2. Mwl. Alexius R. Kagunze | Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) |
| 3. Mhe. Zamda S. Mwebea | Naibu Meya |
| 4. Mhe. James M. Matinde | Mjumbe |
| 5. Mhe. John P. Kisandu | Mjumbe |
| 6. Mhe. Picca N. Chogero | Mjumbe |
| 7. Mhe. Sheilla D. Mshandete | Mjumbe |
| 8. Mhe. Victor T. Mmanywa | Mjumbe |
| 9. Mhe. Moshi H. Kanji | Mjumbe |
| 10. Mhe. Hassan R. Mwendapole | Mjumbe |
| 11. Mhe. Msabila M. Kulwa | Mjumbe |
| 12. Mhe. Zuhura Waziri | Mjumbe |
| 13. Mhe. Juma M. Nkwabi | Mjumbe |
| 14. Mhe. Reuben N. Kitinya | Mjumbe |
| 15. Mhe. Mussa E. Andrea | Mjumbe |
| 16. Mhe. Mariam L. Nyangaka | Mjumbe |
| 17. Mhe. Paschazia C. Seni | Mjumbe |
| 18. Mhe. Peter J. Kwoliba | Mjumbe |
| 19. Mhe. Victor Y. Mkwizu | Mjumbe |
| 20. Mhe. Esther F. Makune | Mjumbe |
| 21. Mhe. Ezekiel J Sabo | Mjumbe |
| 22. Mhe. Enock C. Lyeta | Mjumbe |
| 23. Mhe. Reuben M. Dotto | Mjumbe |
| 24. Mhe. Gulamhafeez Mukadam | Mjumbe |

## B. WASIOHUDHURIA

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Patrobas Katambi (MB) | Kwa taarifa |
| 2. Mhe. Lucy Mayenga (Mbunge VM) | Kwa taarifa |

**C. WATAALAM**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Pius M. Sayayi | Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu. |
| 2. | Kuchibanda K. Snatus | Mkuu wa Kitengo cha Usafi wa Mazingira na Udhibiti taka |
| 3. | Charles Luchagula | Mkuu wa Kitengo cha Utamaduni na Sanaa |
| 4. | Mensaria Mrema | Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu |
| 5. | Naely Elias | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji |
| 6. | Lenard Chepe | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 7. | Eng Kassim Thadeo | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijiji na Miji. |
| 8. | CPA Peter Tarimo | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. |
| 9. | Peres Kamugisha | Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii. |
| 10. | JaneRose Francis | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira. |
| 11. | Mary S. Maka | Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 12. | Lucas Mzungu | Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari. |
| 13. | Octavina Kiwone | Mratibu TASAF |
| 14. | Jacob Mwinuka | Afisa Ardhi Mteule wa Ofisi ya Ardhi Manispaa. |
| 15. | Simon Shoo | Kny ya Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 16. | Dr Elisha Robert | Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe. |
| 17. | Samson S. Nyanda | Kny: Mthibiti Ubora wa Shule. |
| 18. | Lucy Sewe | Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi |
| 19. | CPA Kishenyi Mulokozi | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 20. | Adv. Rose Matunda | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria. |
| 21. | CPA Sunday Nkwambi | Mhasibu wa Mapato |
| 22. | Michael Makotwe | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Usimamizi na Ufuatiliaji |

**D. WAALIKWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Fabian Kamoga | - | For RAS |
| 2. | SSP Kizito M. Kunabi | - | DPO |
| 3. | LTCoL Ford Mwakasege | - | MJA |
| 4. | ASI- Elizabeth G. Kaka | - | Ag. DLP |
| 5. | Insp. Edward Seleman | - | Ag. DFO |
| 6. | Baraka Bulmongmo | - | LGO |
| 7. | Mohamed Doo | - | AG. DBC |
| 8. | Anold Makombe | - | M/Kiti CCM (W) |
| 9. | Hamisa S. Chacha | - | Katibu CCM (W) |
| 10. | Samwel Jackson | - | Katibu wa Mbunge |
| 11. | Haruna Myuyi | - | DSO |

**E. WAKUU WA TAASISI**

1. Eng. Daniel Ojwando - TEMESA
2. Rogath Roghasian - RUWASA
3. John Mtemi - TANESCO
4. Eng.Kulwa E. Maige - TARURA
5. Eng. Uswege Musa - SHUWASA

**F. WATENDAJI WA KATA**

1. Gaudiozi K. Mwombeki - Mtendaji wa Kata ya Ngokolo
2. Fortunatus L. Jilala - Mtendaji Kata ya Chamaguha
3. Elizabeth S. Mbate - Kny Mtendaji wa Kata ya Kolandoto
4. Adella Mukinga - Mtendaji wa Kata ya Kizumbi
5. Joshua Masengwa - Mtendaji wa Kata ya Ndala
6. Mwakaluba Jacob - Mtendaji wa Kata ya Old Shinyanga
7. Costantine M. Masalu - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Masekelo
8. Mahiba Pastory - Mtendaji wa Kata ya Lubaga
9. Abdul Kumalija - Mtendaji wa Kata ya Mwawaza
10. Simon Mashishanga - Mtendaji wa Kata ya Mjini
11. Patrick M. Dotto - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata
12. Mayala Ibrahim - Mtendaji wa Kata ya Kitangili
13. Michael Joshua - Mtendaji wa Kata ya Mwamalili
14. Sarah Wankuru - Mtendaji wa Kata ya Kambarage
15. Emilini Mtambu - Mtendaji wa Kata ya Ndembezi
16. Antony Charles - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibadakuli
17. Ponsian Ngodita - Mtendaji wa Kata ya Chibe

**F: AFISA TARAFA**

1. Telezia K. Alois - Afisa Tarafa ya Mjini
2. Gregory Kachira - Afisa Tarafa ya Ibadakuli
3. Neema Mukandala - Afisa Tarafa ya Old Shinyanga

**G: WAANDISHI WA HABARI.**

1. Hellen B. Mainda - MCL. (Mwananchi)
2. Eunice Kanumba - Jambo FM
3. Stella Ibengwe - Habari leo
4. Mapuli Misalaba - Nipashe
5. Elizabeth Charles - Star TV
6. Elias Gamaya - Afisa Habari Shinyanga Manispaa
7. Boaz Martine - Afisa Habari RS
8.

**SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Esther Daudi | Mwandishi wa Vikao (CC) |
| 2. | Macelina Bwathondi | Mwandishi wa Vikao (CC) |
| 3. | Damaris Charles | Mwandishi wa Vikao (CC) |
| 4. | Amina Juma | Mwandishi Mwendesha Ofisi (MMO) |

**Agenda za kikao zitakuwa kama ifuatavyo: -**

**Siku ya Kwanza tarehe 31.10.2024**

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Agenda za Mkutano.
3. Kupokea na kujadili taarifa za kwenye Kata kutoka kwa Madiwani wa Kata husika pamoja na majibu ya changamoto za Kata kwa kipindi cha robo ya nne.
4. Kuahirisha kikao

**Siku ya Pili tarehe 01.11.2024**

5. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kawaida wa tarehe 29- 30.07.2024.
6. Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024
   - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI tarehe 12.07.2024
   - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 16.07.2024
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe 15.07.2024
   - Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 19.07.2024, 26.08.2024 na 20.09.2024.

7. Kupokea taarifa za utekelezaji wa Idara mbalimbali za Kamati za kudumu kwa robo ya kwanza 2024/2025.
   - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
   - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
   - Kamati ya Fedha na Utawala
8. Taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kama zipo.
9. Masuala ya Kiutumishi.
10. Kufunga Kikao.

**AGD Na.01:2024/25** **MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

**Kumb: BAR.01.1.1** Wajumbe hawakuwa na maswali ya papo kwa papo hivyo, maswali hayo hayakuulizwa.

**AGD Na.01:2023/24** **KUFUNGUA MKUTANO**

**Kumb: BAR.01.3.1** Mwenyekiti alifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya kwanza saa 05.20 Asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe, Kamati ya Ulinzi, Waandishi wa Habari na Wananchi katika Mkutano wa Baraza la Madiwani.

**AGD Na.01: 2023/24** **KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 31. 10 - 01 .11. 2024.**

**Kumb: BAR.01.4.1** Jumla ya agenda 10 zilithibitishwa kwenye Mkutano wa Kawaida wa wa Baraza la Madiwani.

**AGD Na.03 :2023/24:** **KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KWENYE KATA KUTOKA KWA MADIWANI WA KATA HUSIKA.**

**Kumb: BAR.02.5.1** Wajumbe waliwasilisha taarifa za Kata zote 17 kwa kuelezea mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo katika Kata zote. Ilielezwa kuwa changamoto nyingi katika Kata zinajirudia hivyo inahitajika kupata utatuzi wa kudumu. Pamoja na changamoto zilizowasilishwa zilizooneka kuainishwa katika Kata zote ni kama zifuatazo;

- Upungufu wa matundu ya Vyoo katika baadhi ya Shule
- Kutokamilika kwa miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Kata.
- Upungufu wa Wataalam wa Kada mbalimbali katika Kata.
- Miundombinu mibovu ya Barabara hususani Barabara za Mitaa

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe waliipongeza Menejimenti kwa kutatua changamoto nyingi katika Kata na kwa kutekeleza Miradi mingi ya Maendeleo inayoendelea kutekelezwa.

Aidha, walisisitiza kuwa changamoto ambazo hazijapatiwa ufumbuzi ziendelee kufanyiwa kazi hususani upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za Msingi na Sekondari kwa kuwa uliwekwa mpango wa kujengwa kwa awamu.

Pia Wakuu wa taasisi kuchukua changamoto zinazowahusu na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Katibu aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani kwa kuwasilisha mafanikio na changamoto kutoka katika Kata zao na alieleza kuwa Changamoto zote zilizowasilishwa zinafanyiwa kazi kwa kuwa miradi mingi inaendelea kutekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani hususani ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika Shule za msingi na Sekondari.

**AGD Na.04 :2023/24:** **KUAHIRISHA KIKAO**

**Kumb: BAR.02.6.1** Kikao cha kujadili taarifa za Kata kiliahirishwa saa 07:27 mchana

**SIKU 2** **01.11.2024**

**AGD Na.06:2023/24:** **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 29- 30.07.2024.**

**Kumb: BAR.02.7.1** Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 29-30.07.2024 ulisomwa ukurasa kwa ukurasa na wajumbe kuridhia kuwa yaliyomo ndiyo yaliyojadiliwa na hivyo ulithibitishwa na kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kusaini Muhtasari huo.

**AGD Na.06:2023/24:** **KUPOKEA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU YA ROBO YA KWANZA 2024/2025**

**Kumb: BAR.02.8.1** Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya nne ya mwaka 2024/2025 ambayo tayari ilithibitishwa katika vikao vya Kamati vilivyofanyika,

- Kamati ya Kudhibiti UKIMWI wa tarehe 12.07.2024
- Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 16.07.2024
- Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe 15.07.2024
- Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 19.07.2024, 26.08.2024 na 20.09.2024.

**Kumb: BAR.02.8. 2** Wajumbe waliipokea Mihtasari ya Kamati za kudumu na kuridhia kuwa kumbukumbu halali ya vikao vya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

**AGD Na.07:2023/24:** **KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA DIVISHENI MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA KWANZA 2024/2025**.

**Kumb: BAR.02.9.1** Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Divisheni na Vitengo mbalimbali vilivyo chini ya Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambazo ni Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu, Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Kamati ya Kudhibiti UKIMWI, Kamati ya Fedha na Utawala kwa robo ya kwanza 2024/2025 iliwasilishwa kwa Wajumbe.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili.

**Kumb: BAR.02.9.2** **Taarifa ya Kamati ya Kudhibiti Ukimwi**

Taarifa hii iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa, Shughuli za kudhibiti Ukimwi zimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni shughuli

zisizo za tiba na shughuli za tiba. Ilielezwa kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya Julai hadi Septemba, 2024 shughuli mbalimbali zilitekelezwa.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuipitisha.

**Kumb: BAR.03.9.3** **Taarifa ya Kamati ya Mipango Miji na Mazingira**

Taarifa hii iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza ya Julai – Septemba, 2024/2025 Vitengo vilivyo chini ya Divisheni ya Miundombinu na maendeleo ya Vijiji na Miji inayohusisha Vitengo vya ujenzi, Mazingira na Ofisi ya Ardhi na Mipango vilitekeleza shughuli za ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo katika shule za Msingi na Sekondari.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa.

**Kumb: BAR.02.9.4** **Wajumbe walihoji kuwa ni lini Halmashauri itafungua barabara za Kata ikizingatiwa mvua zimeanza kunyesha na Barabara nyingi zimeharibika.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa, suala la ufunguzi wa barabara lipo kwenye mpango na bajeti ya mwaka 2024/2025, na kwa kuwa mwaka wa fedha haujaisha utekelezaji utaendelea kwa awamu kwa kila Kata.

**Kumb: BAR.02.9.5** **Hoja kuhusu wananchi waliopimiwa Ardhi ni lini watapewa namba za viwanja vyao?**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa namba za viwanja zimeanza kutolewa katika maeneo ya Ndala, Mwabundu, Dome, Mageuzi, Kolandoto,Ihapa, Old Shinyanga, Bondeni, Bushushu na Kalonga. Hata hivyo zoezi la ugawaji wa namba linaendelea katika maeno mengine.

**Kumb: BAR.02.9.6** **Wajumbe walihitaji ufafanuzi kuhusu mpango uliopo wa kufanya matengenezo ya Barabara ya kuelekea Dampo.**

Ufafanuzi ulitolewa na Meneja wa TARURA kuwa, barabara ya Dampo haikuwekwa kwenye mpango wa matengenezo ya barabara kwa robo ya pili.

Wajumbe walipokea majibu na kusisitiza kuwa jambo hilo lichukuliwe kwa uzito kwa kuwa Barabara hiyo ni ya muhimu sana hivyo iliagizwa kuwa kufikia tarehe 04.11.2024 wawasilishe taarifa kuhusu barabara hiyo.

**Kumb: BAR.02.9.7** **Hoja kuhusu zoezi la Upandaji Miti.**

Wajumbe walihitaji kujua mpango uliopo kuhusu ugawaji na upandaji miti hasa Katika kipindi hiki cha mvua.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa, Halmashauri imejipanga kugawa miti 5000 kwa ajili ya kupanda katika maeneo mbalimbali kwenye shule, Hospitali na Ofisi mbalimbali.

**Kumb: BAR.02.9.8** **Hoja kuhusu eneo Ibinzamata (Jirani na Soko la Ibinzamata)**

Wajumbe walihitaji kujua endapo Halmashauri imeingia mkataba na mtu binafsi kwa ajili ya kuliendeleza au limemilikishwa.

Ufafanuzi ulitolewa Eneo hilo lilifanyiwa uthamini mwaka 2018 kwa wananchi 400 na kuleta gharama ya Sh 498,500,000 lakini baadae mwaka 11.01.2023 eneo lilipunguzwa na kufidiwa wananchi wachache (10) kwa kulipwa kiasi cha Sh 13,699,745.likiwa na ukubwa wa ekali 6.55

Hata hivyo sehemu ya eneo lililo Jirani na Soko la Ibinzamata limetolewa kwa waombaji kwa ajili ya uwekezaji.

Wajumbe walipokea maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa na Menejimenti.

**Kumb: BAR.02.9.9** **Taarifa ya Uchumi, Afya na Elimu.**

Taarifa ya Uchumi, Afya na Elimu iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2024 Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu ilitekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya kikao chake cha tarehe 17.10.2024 kilichojikita kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizofanyika katika Divisheni na Vitengo zilizo chini ya Kamati hii

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa

**Kumb: BAR.02.9.10** **Hoja kuhusu Shamba la Halmashauri lillilonunuliwa kwa ajili ya uwekezaji**

Wajumbe walihitaji kujua Halmashauri ina mpango gani wa kuliendeleza shamba hilo ili liweze kuzalisha kwa uhalisia kulingana na gharama zilizotumika kununua shamba hilo**?**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri ilinunua Shamba hilo kwa Tsh. 60,000,000. Lengo likiwa ni kuendeleza wakulima kupitia vikundi, Kumekuwa na changamoto kwa vikundi hivyo katika uendeshaji ili shamba hilo lizalishe faida.

Mikakati iliyopo ya kuendeleza shamba hilo ni kutengeneza Mashamba darasa ambayo yatatumika kuwaelekeza wakulima kuhusu kuzalisha mazao katika kipindi cha kiangazi ambapo wakulima na Wafanyabiashara watajifunza.

Wajumbe walipokea maelezo ya ufafanuzi na kuelekeza kuwa,kwa eneo hilo ni kubwa baada ya kuandaa shamba darasa eneo litakalobaki uwekwe utaratibu wa namna ya kuwekeza kwa vikundi vinavyojishughulisha na kilimo,visimamiwe ipasavyo na wataalam ili kuwawezesha kujiinua kiuchumi na Halmashauri pia ipate mapato.

**Kumb: BAR.02.9.11** **Hoja kuhusu uendeshaji wa Kiwanda cha Tofali,**

Wajumbe walihitaji kujua ni namna gani Halmashauri imeweka utaratibu wa kupata gawio kutoka katika mradi huu.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa, kiwanda kilipokea fedha za mtaji kutoka Halmashauri, ambapo awali kilipokea Sh. 20,000,000 awamu ya pili kilipokea 27,000,000. Kwa sasa kiwanda kinaendeshwa na Kampuni ambayo inasimamia mradi huo. Kiwanda kinaendelea na uzalishaji tayari kimefanya kazi na baadhi ya Taasisi ikiwemo Mahakama na shule ya Sekondari Rajani,kwa kuwa bado mtaji ni mdogo na baadhi ya taasisi wamekopa matofali hawajalipa fedha

Hivyo kampuni ipewe muda zaidi wa kusimamia uzalishaji ili kutoa matokeo Chanya kwa Halmashauri.

Wajumbe walisisitiza taasisi zote zinazodaiwa na kampuni wafuatiliwe ili warejeshe fedha wanazodaiwa ili kiwanda kiweze kuongeza uzalishaji kwa kuwa lengo ni kupata faida na Halmashauri iweze kupata mapato.

**Kumb: BAR.02.9.12** **Hoja kuhusu Uhaba wa Malisho kwa Wafugaji**

Wajumbe walihitaji kujua elimu ya malisho inatolewa katika Kata zipi kwa kuwa Halmashauri hairuhusu ufugaji holela.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri ilitoa semina kwa wafugaji wa Manispaa/Wilaya ya Shinyanga. Elimu imetolewa kwa kuwa Mji umeendelea kukua na maeneo ya kuchungia yanapungua hivyo wafugaji walielekezwa kuandaa malisho yao ambapo waliitwa pamoja katika ukumbi wa Manispaa na wengine walitembelewa katika maeneo yao (Kata zote zenye wafugaji) kwa kuwakusanya pamoja na kuwapa elimu hiyo

**Kumb: BAR.02.9.13** **Ushauri**

Wakulima katika Kata zenye hadhi ya Kijiji wapewe elimu ya ufugaji ili kuweza kupata uelewa wa Pamoja ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu Madiwani ambao Kata zao zina maeneo ya kilimo,ili wasaidie kutoa elimu hiyo kwa wakulima wa walioko katika maeneo yao.

**Kumb: BAR.02.9.14** **Hoja kuhusu Ukamilishaji wa Madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mwasele**

Wajumbe walihoji ni lini Manispaa ya Shinyanga itakamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule ya Sekondari Mwasele.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa, suala limechukuliwa na kuwekwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya utekelezaji.

**Kumb: BAR.02.9.15** **Hoja kuhusu Utoaji wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulamavu**

Wajumbe walihitaji kujua ni lini Madiwani watapewa Elimu ya utoaji wa mikopo kwa vikundi ili kuwa na uelewa kuhusu utoaji wa mikopo hiyo.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa utaratibu unaofanyika kwa sasa ni kuunda Kamati kuanzia ngazi ya Kata na kutoa Elimu ya utaratibu wa utoaji mikopo kwa kuwa kufikia Mwezi Disemba vikundi vitatu vinavyoendelea na taratibu vitakuwa vimepewa mikopo na hatua inayofuata ni kutoa elimu kwa Waheshimiwa Madiwani kuhusu utoaji wa mikopo ili kujenga uelewa wa pamoja na kuwaelimisha Wananchi katika Kata zao.

**Kumb: BAR.02.9.16** **Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala.**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala iliwasilishwa ambapo wajumbe waliipokea taaifa hiyo na kutoa pongezi kwa wataalam na Wajumbe wa Kamati ya Fedha kwa usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali.

Aidha, walishauri wataalam kuendelea kuelimisha wananchi/Wafanyabiashara kulipia ushuru na tozo mbalimbali pasipo shuruti ili kuepuka kutozwa faini zisizo za lazima.

**Kumb: BAR.02.9.17** **Hoja kuhusu Jeshi la Wananchi Kukusanya Tozo ya Maegesho**

Wajumbe walihoji kuwa, Kambi ya Jeshi wanakusanya tozo ya maegesho ya malori walipataje kibali wakati Sheria ndogo inaelekeza kuwa Halmashauri ndio yenye mamlaka na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya maegesho.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa mazungumzo yatafanyika na viongozi wa Jeshi ili kujua wanatumia Sheria ipi kukusanya tozo hiyo.

**Kumb: BAR.02.9.18** **Hoja kuhusu Uuzaji wa Viwanja vya Halmashauri**

Wajumbe walihitaji ufafanuzi kuhusu uuzaji wa viwanja kwa kuwa wananchi wengi hawafahamu viwanja hivyo vinapopatikana Hali inayopelekea viwanja hivyo kutouzwa kwa wakati.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa viwanja vinatangazwa katika Kata, gari la Matangazo linapita katika maeneo mbalimbali ya Kata. Hata hivyo matangazo yataendelea kutolewa kwakuwa wateja/wanunuzi wengi ni Watumishi. Aidha ununuzi wa viwanja vinategemea na uhitaji kwa kuwa watu wengi wakinunua viwanja kwa mara moja, uhitaji unakuwa sio mkubwa.

**Kumb: BAR.02.9.19** **Wajumbe walihoji kuhusu idadi ya viwanja vilivyouzwa kwa robo hii**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa, kwa robo hii ya kwanza vimeuzwa viwanja 33 vyenye thamani ya Sh. 94 Milioni. Aidha ilielezwa kuwa, mradi wa kupima, kupanga na kurasimisha unaendelea katika maeneo ya Airport, Ibadakuli, Dome, Mwadui, Butengwa na Nhelegani Halmashauri ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 1 na milioni 128.

**Kumb: BAR.02.9.20** **Hoja kuhusu Makusanyo ya Ushuru wa bajaji na Pikipiki**

Wajumbe walihoji kuhusu ushuru wa Bajaji na pikipiki kwa kuwa mapato yake hayajaainishwa kwenye taarifa.

Ufafanuzi ilitolewa kuwa ushuru wa Bajaji na Pikipiki unakusanywa na LATRA kisha inawasilisha asilimia 20 ya mapato yaliyoelekezwa Halmashauri.
Baada ya majadiliano wajumbe waliazimia kuwa;

**Kumb: BAR.02.9.21** **MAAZIMIO:**

- Menejimenti ifanye ufuatiliaji kuhusu Jeshi la wananchi kukusanya mapato ya ushuru wa Maegesho.

  Azimio limezingatiwa, Majibu yaliwasilishwa kwenye Kamati husika na kujadiliwa).

- Meneja wa TARURA awasilishe taarifa ya matengenezo ya Barabara ya kuelekea Dampo.kwa Mkurugenzi

  Azimio limezingatiwa,Taarifa iliwasilishwa kwa Mkurugenzi kwa barua yenye kumb.No.AG.199/366/01C/38 ya tarehe 20.01.2025 ya kueleza kuhusu kuomba fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ikiwa ni pamoja na Barabara zote ambazo zimeharibika kipindi cha mvua, kinachosubiriwa ni ridhaa ya kutangaza zabuni.

- Kuanzisha Stendi ya Hiace katika eneo lililokua machinjio ya zamani
  Azimio limezingatiwa, Majibu yaliwasilishwa kwenye Kamati husika na kujadiliwa.

**AGD Na.08:2023/24:** **TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI.**
**Kumb: BAR.01.10.01** **Taarifa za Taasisi**

**(a) SHUWASA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kuongeza mtandao wa Maji safi katika maeneo ya Manispaa ya Shinyanga kupitia vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwa ni pamoja na mapato ya ndani ya Mamlaka, Serikali Kuu na Wafadhili. Aidha SHUWASA inatekeleza awamu ya pili ya Mradi wa Usafi wa Mazingira kupitia program ya Investment Financing Facility – Out Based Aid Programme (IFF – OBA). Mradi huu unahusisha upanuzi wa Mtambo wa kuchakata tope kinyesi uliopo Kizumbi- Nhelegani kutoka lita 40,000 hadi 100,000 kwa siku, Pia Mradi unahusisha ununuzi wa gari la kunyonya na kusafirisha maji taka lenye ujazo wa lita 10,000. Mradi umeanza kutekelezwa tarehe 25.03.2024 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 12 kwa gharama ya Sh. 817,183,266.00.

Aidha, Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga inatekeleza mradi mkubwa kupitia fedha za mkopo wa riba nafuu toka Shirika la Maendeleo la Ufaransa (French Development Agency; AFD) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania. Mradi huu wenye thamani ya EURO milioni 76 (Takribani TZS Bilioni 195) unahusisha kazi zifuatazo; -

i. Ujenzi wa mtandao wa Maji safi wenye urefu wa kilomita 287
ii. Ukarabati wa mtandao chakavu wa Maji safi unaofikia kilomita 100.

iii. Ujenzi wa tanki moja la kuhifadhia maji lenye ujazo wa mita za ujazo 1,500 katika kata ya Kolandoto
iv. Ujenzi wa mitambo miwili ya kuchakata tope kinyesi (Ihapa, Mwagala);
v. Ukarabati mkubwa wa mtambo wa kutibu Maji safi Ning'hwa na tathimini ya ufanisi wa bwawa la Ning'hwa
vi. Ujenzi wa Jengo jipya la Ofisi.

**Kumb: BAR.01.10.02**

Baada ya taarifa kuwasilishwa, Wajumbe walipongeza taasisi hiyo kwa ajili ya mradi mkubwa watakaoutekeleza kama ilivyowasilishwa kwenye taarifa, Aidha, walisisitiza kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi Miundombinu ya maji itakayowekwa izingatie maeneo yaliyopimwa (viwanja).

Ufafanuzi ulitolewa kuwa kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi utanyika uhakiki wa maeneo yatakayopitiwa na mradi huo hivyo suala hilo litazingatiwa.

Ilisisitizwa kuwa SHUWASA kuhamisha mabomba yasikatwe wakati wa matengenezo ya Barabara na kufanya ukarabati wa Miundombinu ya mabomba hasa ya zamani kwa kuwa miundombinu yake imekuwa mibovu ambapo baadhi ya wananchi wanalalamika kuhusu uvujaji wa maji katika mabomba.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa SHUWASA inao utaratibu wa kufanyia matengenezo kila mara mabomba yanapoharibika, kufanya ukarabati wa kubadilisha miundo mbinu iliyochakaa hivyo suala hili ni sehemu ya shughuli za taasisi za kila siku.

**Kumb: BAR.01.10.03**

**Hoja kuhusu Bili kubwa za Maji kwa baadhi ya maeneo ndani ya Manispaa**

Wajumbe walieleza kuwa kuna baadhi ya wananchi wanalalamika kuletewa bili kubwa za maji tofauti na matumizi yao.
Ufafanuzi ulitolewa kuwa suala hili limepokelewa na litafanyiwa kazi kwani taasisi ina utaratibu wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mtandao wa Maji.

**Kumb: BAR.01.10.04**

**(b) TARURA**

Taarifa ya utekelezaji wa miradi inayoendelea ya matengenezo ya Barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ina mtandao wa barabara wenye urefu wa Km780.184, kilometa 193.635 ni barabara zinazounganisha kata na kata pia zinaunganisha Tarafa na Wilaya Jirani (Collector Roads), Kilometa 585.549 ni

barabara zinazounganisha kata na Kijiji (Feeder Roads). Aidha Halmashauri ina mtandao wa kilometa 22.972 za lami, kilometa 210.328 za changarawe na kilometa 546.884 za Udongo. Ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 TARURA Manispaa ya Shinyanga imetengewa jumla ya **Tshs. 2,928,035,000.00,** katika fedha hizi, fedha za matengenezo ya barabara ni Tshs. **1,428,035,000.00,** fedha za jimbo ni **Tshs. 500,000,000.00** na fedha za tozo ya mafuta ni **Tshs. 1,000,000,000.00**

Aidha hadi sasa TARURA imepokea jumla ya **Tshs. 27,620,000.00** sawa na **Asilimia 1.93%.** Ilielezwa kuwa, TARURA Manispaa ya Shinyanga inaendelea na utekelezaji wa miradi ya matengezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo jumla ya miradi/Mikataba miwili (02) yenye jumla ya **Sh. 780,819,610.00 inatekelezwa**.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuipongeza taasisi hii kwa kazi nzuri wanazozifanya na walitoa wito kwa taasisi hii kufanya marekebisho ya barabara katika maeneo yaliyoharibika ndani ya Manispaa hasa kipindi hiki cha masika.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa.Matengenezo yanaendelea ikiwa ni pamoja na matengenezo ya Madaraja kwa barabara zilizoharibika wakati wa mvua. Hata hivyo fedha za dharura zimeombwa kwa ajili ya matengenezo.

**AGD Na.09:2023/24:** **MASUALA YA KIUTUMISHI**

**Kumb: BAR.01.11.01**

Taarifa ya masuala ya Kiutumishi iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa Watumishi sitini na sita (66) waliopendekezwa kuthibitishwa kazini pamoja na watumishi sabini na mbili (72) wa Divisheni na Vitengo katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga walipendekezwa kuthibitishwa vyeo vya Muundo baada ya kumaliza muda wa majaribio.

Baada ya taarifa kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea na kuwathibitishwa Watumishi sitini na sita (66) kazini baada ya kumaliza mwaka kama ilivyo utaratibu kwamba Mtumishi anapoajiriwa sharti atimize miezi 12 ndipo athibitishwe kazini pamoja na Watumishi sabini na mbili (72) kuthibitishwa kwenye vyeo vya Muundo baada ya kumaliza muda wa matazamio.

**AGD Na.10:2023/24: KUFUNGA MKUTANO**
**Kumb: BAR.01.12.01 Nasaha za Viongozi**

- Kupongeza Baraza la Madiwani kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia ukusanyaji wa mapato na utekekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Kushukuru hali ya utulivu ndani ya Baraza hivyo ushirikiano uendelee ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa Manispaa ya Shinyanga.

Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 8:54 mchana kwa kuwashukuru Wajumbe, waalikwa, Waandishi wa Habari, Wananchi pamoja na Wataalam kwa kushiriki vizuri Mkutano wa Baraza la Madiwani.

**KUMBUKUMBU HIZI ZIMETHIBITISHWA NA**

| ________________________ | ________________________ |
|---|---|
| Mwl Alexius R. Kagunze | Mhe. Elias R. Masumbuko |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE**_________________

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 01.11.2024**

| AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| **AGD Na.07:2023/24: KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA DIVISHENI MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA KWANZA 2024/2025**. **AZIMIO;** Menejimenti ifanye ufuatiliaji kuhusu Jeshi la wananchi kukusanya mapato ya ushuru wa Maegesho. | **Katibu wa Baraza** | Azimio limezingatiwa, Majibu yaliwasilishwa kwenye Kamati husika na kujadiliwa). |
| **AZIMIO;** TARURA kuwasilisha taarifa kwa Mkurugenzi kuhusu matengenezo ya Barabara ya kuelekea Dampo. | **Katibu wa Baraza** | Azimio limezingatiwa,Taarifa iliwasilishwa kwa Mkurugenzi kwa barua yenye kumb.No.AG.199/366/01C/38 ya tarehe 20.01.2025 ya kueleza kuhusu kuomba fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ikiwa ni pamoja na Barabara zote ambazo zimeharibika kipindi cha mvua, kinachosubiriwa ni ridhaa ya kutangaza zabuni. |
| **AZIMIO;** Kuanzisha Stendi ya Hiace katika (eneo lililokua machinjio ya zamani | **Katibu wa Baraza** | |